



## TAARIFA KWA UMMA

### KUHUISHA TAARIFA ZA MAKAMPUNI NA MAJINA YA BIASHARA NDANI YA SIKU 90

Dar es Salaam, 27 Septemba 2019

Hii ni kuutarifu umma kuwa WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI (BRELA) inaendelea na zoezi la uhuishaji wa Taarifa za makampuni yaliyosajiliwa nje ya mfumo wa kielektroniki. Tunapenda kutoa taarifa kwa umma na watu wote wenye makampuni na Majina ya Biashara kuhakikisha wanauhisha taarifa za makampuni yao na Majina ya Biashara katika kipindi cha SIKU 90 kuanzia tarehe ya tangazo hili.

#### MAHITAJI NA TARATIBU ZA UHUISHAJI WA TAARIFA

- Muombaji awe na Namba ya kitambulisho cha cha Utaifa (NIN) ambayo husaidia kufungua akaunti ya BRELA kwenye tovuti ya Wakala
- Endapo maombi ni ya kampuni unatakiwa kuwa na Namba ya utambulisho wa Mlipa Kodi (Tax Identification Number (TIN) ya kila Mkurugenzi na ya Kampuni husika.
- Kupitia taarifa za kampuni na kuhakikisha zipo sahihi kisheria na kikanuni
- Kujaza 'consolidated form' katika mfumo wa ORS na kupakia taarifa zozote zinazohitajika mfano Taarifa ya Mwaka (Annual

returns), mabadiliko yaliyotokea katika kampuni ambayo hayakuletwa hapo awali

- Kuweka saini katika fomu zote, kuweka saini kwenye 'consolidated form', kuzipakia katika akaunti na kutuzima BRELA kwa njia ya mtandao.
- Baada ya kukamilisha kuhuisha (updated) taarifa itahakikiwa na kupatiwa ankara ya malipo na muombaji atatakiwa kulipia benki au kwa njia ya simu.

#### **KATIKA ZOEZI HILI BRELA INASISITIZA MAMBO YAFUATAYO:**

Wakati zoezi hili linaendelea BRELA inapenda kutoa kwa kifupi taratibuza namna ya kutumia huduma za BRELA kwa njia ya mtandao

- Kuwasilisha taarifa sahihi zinazoendana na taarifa zilizopo katika masijala ya usajili.
- Kufanya zoezi wenyewe au kuwatumia wenye weledi na uelewa wa kutosha wa sheria za sajili mbalimbali.
- Kuwasilisha taarifa zilizokamilika
- Kuzingatia maelekezo ya marekebisho kwenye maombi yanayorudishwa kwao.
- Kuambatisha nyaraka sahihi kwa kampuni zenye mabadiliko mbali mbali.
- Kutorudia kosa lile lile au kuongeza makosa mengine baada ya kupewa maelekezo ya masahihisho.
- Kutoa taarifa za kweli na uhakika na kuzingatia marekebisho wanayopewa ili kuleta ufanisi na uharaka.

- Kuhakikisha kuwa anayefungua akaunti kwenye mfumo wa ORS wa BRELA ni Mmiliki wa hisa katika Kampuni au Mwenye jina la biashara na pia unashauriwa kutunza Jina na neno la siri (User name na password).

Imetolewa na:



**KAIMU AFISA MTENDAJI MKUU  
WAKALA YA USAJILI WA BISHARA NA LESENI (BRELA)  
JENGO JIPYA LA USHIRIKA, MTA A WA LUMUMBA**

**S.L.P. 9393,**

**DAR ES SALAAM.**

Simu: +255-22-2181344, 2180113, 2180141, 2180048,  
Nukushi: +255-22-2180371  
Baruapepe: [usajili@brela.go.tz](mailto:usajili@brela.go.tz); [ceo@brela.go.tz](mailto:ceo@brela.go.tz)  
Tovuti: [www.brela.go.tz](http://www.brela.go.tz)